

JINSI YA KUPATA LESENI YA BIASHARA WILAYA YA ULANGA.

1. Mteja anatakiwa kufika katika ofisi ya biashara na kueleza shughuli anayotaka kuifanya na mahali anapotaka kufanyia hiyo biashara.
2. Mteja anatakiwa kujaza fomu ya maombi ya leseni ya biashara(TFN 211) au fomu ya maombi ya leseni ya vileo.
3. Baada ya kujaza taarifa zake kwenye fomu ya maombi ya leseni ataenda TRA kwa ajili ya kufanyiwa makadilio ya kodi ya mapato kulingana na biashara anayotaka kuifanya na endapo atakua hana TIN atapatiwa hapo.
4. Baada ya kulipa kodi ya mapato atapewa TIN pamoja na TAX CLEARANCE CERTIFICATE.
5. Mteja atarudi ofisi ya biashara kwa ajili ya kuingiza taarifa zake kwenye mfumo wa KIELECTRONIC (Local Government Revenue Collection Information System) kupewa hati ya madai (Invoice)kwa mujibu wa muongozo wa viwango vya wizara ya viwanda na biashara kulingana na aina ya biashara,eneo na hali ya biashara (kama ni shina au tawi).
6. Mteja huenda benki kwa ajili ya kulipa fedha (benki ya NMB)
7. Fedha ikishalipwa benki huenda ofisi ya fedha kupata stakabadhi ya ada ya kawaida (General Receipt).
8. Akishapata stakabadhi hurudi ofisi ya biashara na kupewa leseni yake.Aidha mteja hupewa maelekezo ya namna ya matumizi ya leseni yake na muda wa kuisha leseni hiyo.